nawe kila siku. Unaweza kuongea naye kama vile unavyoongea na marafiki zako.

**Tafuta marafiki Wakristo.** Ushirika utakaopata kutoka kwa wengine waliotoa maisha yao kwa Yesu utakuwa chanzo kikuu cha nguvu za kiroho na kutiwa moyo.

**Weka azimio la kuendelea kumwishia Mungu**. Fanya uamuzi wa kuthamini ushirika ulio nao na Mungu na uupe umuhimu mkubwa kuliko kitu chochote kile. Ijapokuwa inawezekana kumwacha Mungu na kuijitenga naye tena, hilo halina haja ya kutokea. Yeye atakusaidia kuendelea kuwa mwongofu ikiwa hiyo ndiyo shauku yako kubwa.

**Waambie watu wengine juu ya wokovu wako.** Itakuwa vizuri kuwaambia rafiki zako wa karibu. Vilevile tungependa kujua kile alichofanya Mungu katika maisha yako. Unaweza kutuandikia kwa anwani ifuatayo. Unaweza kuomba kutumiwa vijitabu vya bure, viitwavyo, "Anza Maisha Mapya" na "Siku 30 Kuelekea katika Umilele" ili uweze kutiwa moyo zaidi na kupata mwongozo katika maisha yako mapya na Mungu.

**APOSTOLIC FAITH CHURCH**
World Headquarters
5414 SE Duke Street
Portland, Oregon 97206 U.S.A.
www.apostolicfaith.org

SW20-1208

# HATUA ZINAZOELEKEZA KWENYE *Maisha Mapya*

Kwa nini niko hapa? Kwa nini ninahisi kama kuna kitu kinakosekana katika maisha yangu? Je, kuna cha ziada katika maisha mbali na kile ambacho nimekwishakiona? Ni Nini nitakachofanya nitakapokufa?

Kwa wakati mmoja au mwingine, inawezekana umewahi kufikiria juu ya maswali haya. Pengine unasumbuka na swali moja sasa hivi. Huenda kuna wakati fulani ulihisi kwamba umepata majibu, lakini hisia hiyo haikudumu. Kuna kitu kinachokosekana, lakini haujui ni kitu gani au utakipata wapi. Kuna kitu fulani hakiko sawa sawa, lakini haujui jinsi ya kukirekebisha. Kila jibu, kila uhusiano, kila uzoefu hukuacha ukihisi utupu. Kwa hiyo unaendelea kutazama, unaendelea kujaribu, unaendelea kutafuta.

Shida si "kile" unachokikosa. Shida ni "Nani" unayemkosa. Huyo Nani ni Mungu!

Mungu Ndiye aliyekuumba wewe, na alitengeneza mahali ndani yako ambapo yeye tu ndiye anayeweza kupajaza—Nafasi iliyo na ukubwa wa Mungu, inayomsubiri yeye tu.

Mungu si falsafa. Mungu si dhana. Yeye ni Muumba wa mbingu na nchi, na anakupenda sana! Anajua siku yako ya kuzaliwa, anajua kila sehemu ya nafsi yako, kila tukio katika maisha yako hadi kufikia wakati huu, na anajua kile kilicho mbele yako. Kitabu chake, yaani Biblia, kinasema kwamba yeye anajua hata idadi ya nywele zilizo kichwani mwako na mawazo na makusudi ya moyo wako.

Utupu ulio katika moyo wako, kule kuhisi kwamba kuna kitu kinachokosekana, kiko hapo kwa sababu umetenganishwa na Mungu. Utengano huo umesababishwa na dhambi ni kitu kibaya, ni mzizi wa ubinafsi, matendo maovu, na mawazo mabaya. Hivi ndivyo ilivyotokea.

Hapo mwanzo, Mungu alimuumba mwanaume na mwanamke wa kwanza duniani, Adamu na Hawa. Walifurahia kuwa na ushirika kamili na Mungu. Walitembea na kuongea naye, wakiishi, maisha takatifu  na ya furaha katika bustani iliyokimu mahitaji yao yote. Agizo la Mungu kwa Adamu na Hawa ilikuwa ni kutokula matunda ya mti fulani hapo bustanini: mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Sheria hiyo iliwekwa hapo kwa sababu ya upendo aliokuwa nao Mungu juu yao, kwa sababu kufikia wakati huo Adamu na Hawa walijua mema tu, na Mungu alifahamu kuwa kujua mabaya kungewaumiza sana. Hata hivyo, Mungu alikuwa amewaumba na uwezo wa kuchagua kumtii Mungu, nao wakaamua kutomtii. Walikula tunda kutoka kwenye ule mti waliokatazwa na Mungu, na matokeo yake ikawa, dhambi ikaingia mioyoni mwao. Kwa sababu Mungu hana uhusiano wowote na wenye dhambi, dhambi yao iliwatenganisha naye.

Kizazi cha Adamu na Hawa—yaani kila mtu aliyezaliwa katika ulimwengu huu—alirithi dhambi ya asili kutoka kwa babu zake. Badala ya kuja duniani na shauku ya kutenda mema, kila mmoja wetu huzaliwa na mvuto asilia wa kutenda dhambi. Jinsi tunavyozeeka tunafanya machaguo ya kibinafsi ya kutenda dhambi (kutotii sheria ya Mungu). Dhambi inaweza kuwa kitu cha kawaida au kigumu kueleza, lakini wakati wote inatutenganisha na Mungu, na mshahara wa dhambi ni mauti na kutenganishwa na Mungu milele yote.

Tunamshukuru Mungu kwa sababu huo sio mwisho wake.

Mungu anatupenda sana hivi kwamba alitengeneza njia ambayo ingekuwa daraja la kuziba lile pengo la utengano linalotokana na dhambi. Alimtuma Mwanawe pekee, Yesu, ulimwenguni kuishi kama mwanadamu na kulipia gharama ya dhambi zetu. Mshahara wa dhambi ni mauti. Kwa kuwa Yesu hakuwa na dhambi, angeweza kulipia dhambi za wengine, kwa hiyo alikufa msalabani kwa ajili yetu. Kisha, baada ya siku tatu, Yesu alifufuka kutoka wafu na kutembea duniani tena! Jambo hilo la ajabu lilinakiliwa na mamia ya watu waliomuona Yesu baada ya kufufuka kwake. Sasa anaishi Mbinguni na Mungu.

Hata hivyo, kwa kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu haina maana kwamba sasa hatujatenganishwa na Mungu. Kujua juu ya kifo cha Yesu tu hakutoshi. Kila mtu lazima aje kwa Mungu kibinafsi ili aweze kupokea msamaha binafsi wa dhambi.

Unawezaje kumwendea Mungu na kupata msamaha? Katika Biblia, Mungu ameweka hatua ambazo unaweza kuzifuata. Ukichukua kila hatua kwa uwazi na kwa njia ya kweli, atakuhakikishia kwamba umepata msamaha. Ujuzi huo unaitwa wokovu. Mtu anapoupokea wokovu, ile hali ya kutenganishwa na utupu hupotea baada ya muda. Ataanza kuhisi kuwa mkamilifu, kupendwa, na moyo wako utakuwa na amani. Ataanza kumpenda Mungu na watu wengine. Jambo linalothibitisha kwamba hili ni kweli ni wale ambao wameupokea msamaha wa Mungu na maisha yao kubadilishwa kabisa.

Ikiwa unataka kupokea msamaha wa Mungu, hivi ndivyo unavyotakiwa kufanya:

**Kubali kwamba unalo hitaji.** Kubali kwamba umetenda dhambi na kwamba unahitaji msaada wa Mungu. Biblia inatuambia, "kwa sababu wote wametenda dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23). Mtu mmoja ambaye ombi lake limenakiliwa katika Luka 18:13, alisema, "Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi."

**Ungama na utubu.** Sikitika kwa ajili ya zile dhambi ulizotenda na umwombe Mungu akusamehe. Neno la Mungu linatuahidi, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu" (1 Yohana 1:9). Vilevile inasema, "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe," (Matendo 3:19).

**Ziache zile dhambi zako za awali.** Amua kwamba kwa msaada wa Mungu utaziacha dhambi katika maisha yako yote. Tunasoma katika Isaya 55:7, "Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake: Na amrudie Bwana, naye atamrehemu...naye atamsamehe kabisa." Hiyo ni ahadi!

**Mwamini Yesu Kristo.** Kwanza, lazima uamini kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako na kwamba yu hai leo. Kisha baada ya kuzifuata kwa uwazi na kwa njia sahihi hatua zilizotajwa hapo juu, amini kwamba Mungu atasikia ombi lako na kukuokoa. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

**Mkaribishe Yesu Kristo maishani mwako na katika moyo wako.** Unaweza kuwa mtoto wa Mungu leo ikiwa utamwendea kwa moyo wako wote na kufuata hatua hizi kwa moyo wako wote na kujitoa kwake. Omba ombi kama hili kutoka katika kilindi cha moyo wako.

*Mungu, Asante kwa kunipenda. Ninakuja kwako leo nikiamini kwamba Mwanao, Yesu alikufa kwa ajili yangu na kwamba yu hai leo. Ninajua kwamba nimetenda dhambi na kwamba dhambi zangu zi kinyume cha mapenzi yako. Ninataka kuziacha dhambi zangu na kutozirudia tena. Tafadhali nisamehe kwa kila tendo baya au wazo baya ambalo nimewahi kuliwaza. Ninakuomba uingie maishani mwangu uwe Bwana na Mwokozi wangu. Ninachagua kukuishia wewe, na ninakuomba uniongoze maisha yangu yote. Nisaidie kuanzia leo na kuendelea kukutii nakukupendeza wewe. Asante kwa kunisikia na kunijibu hili ombi langu. Katika jina la Yesu, Amina.*

Mungu atakujulisha wakati utakapokuwa umeokolewa. Biblia inatuambia, "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Warumi 8:16). Utasikia furaha na uhuru! Furaha na kuridhika zitachukua nafasi ya hatia, utupu na maumivu ya moyo.

Utakapokuwa na hakika kwamba dhambi zako zimesamehewa na hujatengwa na Mungu tena, utafanya nini tena?

**Chukua nakala ya Kitabu cha Mungu, Biblia.** Anza kwa kusoma Kitabu cha Yohana katika Agano Jipya. Utajifunza juu ya maisha ya Yesu hapa duniani na jinsi alivyokufa kukutengenezea njia na wewe kuweza kuunganishwa naye.

**Anza kuongea na Mungu.** Yeye anataka kusikia kutoka kwako na kutembea pamoja